Makala haya yanahu su matatizo ya kiuhariri katika vitabu vya kiada vya Kiswahili nchini Tanzania. Makala yanalenga kubainisha na kujadili matatizo ya kiuhariri yanayojitokeza katika vitabu vya kiada vya shule za msingi. Uchunguzi wa kubainisha makosa haya unachochewa na kuwapo kwa malalamiko mengi ya kiufundi katika tasnia ya uchapishaji, kwani baadhi ya tafiti zimeeleza kwa ufupi sana kero zinazojitokeza katika vitabu (Thonya 1993 na Nkata 1993). Uchunguzi wa maktabani umetumika katika kupata makosa, ambapo tumeweza kusoma, kutathmini na kuhakiki vitabu vinne vya kiada vya Kiswahili vya shule za msingi. Maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Maktaba Kuu na ile ya TATAKI pamoja na makavazi ya TATAKI zimehusika. Nadharia ya “mawazo ni ya mwandishi, kitabu ni cha mhariri” ilitumika. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ambapo data na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo, majedwali na vielelezo. Makalaaya yamegundua kuwapo kwa makosa mengi ya kiuhariri katika vitabu vya kiada vya Kiswahili nchini Tanzania. Kwa mfano, makosa ya matumizi ya herufi kubwa, vifupisho na finyazo, upangiliaji wa vichwa vya habari na makosa ya istilahi. Kwa kuwa makala haikusudii kutoa sababu za kuwapo kwa makosa hayo kwa hiyo haitakuwa sehemu ya mjadala.

Juma, Mwanahija A. • Baraza la Kiswahili la Zanzibar (Bakiza) • mwanahijajuma123@gmail.com  
Said, Amour S. • Baraza la Kiswahili la Zanzibar (Bakiza) • amosaid2004@yahoo.com

## **ULINGANISHI WA VISAWE NA VIBADALA VYA LAHAJA ZA KISWAHILI ZA ZANZIBAR**

### **Ikisiri**

Lahaja ya Kimakunduchi huzungumzwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya kusini mwa Kisiwa cha Unguja. Ni lahaja ambayo ina msamiati mwingi wa asili ya lugha za Kibantu ukilinganisha na Kiunguja mjini ambacho kimeathiriwa na mwingiliano wa watu unaotokana na biashara au utawala, jambo ambalo limesababisha kuingia kwa msamiati mwingi wa Kiarabu na Kiingereza. Kitumbatu ni lahaja inayozungumzwa kwa kiasi kikubwa kaskazini ya kisiwa cha Unguja hususan Tumbatu. Lahaja hii inafananishwa na Kimakunduchi kwa kuwepo kwa mlingano wa baadhi ya msamiati. Kipemba ni lahaja inayozungumzwa kwa kiasi kubwa katika kisiwa cha Pemba. Ni lahaja yenye kujitofautisha na lahaja nyengine za Kiswahili kwa matumizi ya sauti /n/ kuliko lahaja nyengine za Zanzibar. Kiungujamjini ni lahaja inayozungumzwa kwa kiasi kikubwa mjini Unguja . Hii ni lahaja iliyoteuliwa na kusanifishwa hatimae kuwa Kiswahili Sanifu. Makala hii inatarajia kulinganisha visawe na vibadala vya lahaja za Zanzibar Kimakunduchi, Kitumbatu,Kipemba na Kiungujamjini . Vipengele vilivyoshughulikiwa ni mfanano na tofauti za maumbo ya visawe na vibadala vya lahaja hizo. Aidha makala hii imeonesha matumizi ya maneno katika muktadha halisi wa matumizi.

Kame, Mbwarali • Moi University (Eldoret), Kenya  
dktabuyaasir@gmail.com

## **USHAIRI WA WASWAHILI KARNE YA ISHIRINI NA MOJA MUINGILIANO WAKE NA USHAIRI WA KIARABU**

### **Ikisiri**

Waswahili wa mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki wamesifika na uimbaji wa ushairi kwenye muktadha mbai mbali, tumbuizo za Kiswahili husheheni arudhi tofauti tafauti zikiwemo za asili ya Kiswahili pia zikichukua mitindo ya Waarabu kwenye uimbaji. Makala hii itaangazia Uimbaji wa mashairi ya Kiswahili yanavyoimbwa kwenye karne ya ishirini na moja tukipigia mfano ushairi unaoimbwa na *Mahmuud Mau* na *Ahmed Sheikh Nabahani* wote wawili wakiwa na asili ya mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki na wakiwa na chembechembe za Kiarabu na waliosifika kwenye uimbaji wa mashairi ya Kiswahili karne ya 21. Mifano tofauti tofauti yenye kufanana baina ya tumbuizo za Kiswahili na Kiarabu zitaangaziwa kwenye waraka huu pia suala la arudhi zinazo tumika kwenye tumbuizo za lugha mbili zitafafanuliwa.

## **THE 21ST CENTURY SWAHILI POEM INTARUCTION WITH ARABIC POEM**

### **Abstract**

Swahili coastal people in East African have been characterized by the singing of poetry in different context, the Swahili poem is loaded with different singing styles in different variations Swahili traditional and Arabs included, This article will review the singing of Swahili poetry in the twenty-first century by giving example of *Mahmuud Mau* and *Ahmed Sheikh Nabahani* poetry, both of whom originated from East Coast of Africa with some Arab impacts among them in singing of Swahili poetry 21st century. Different models of singing style between Swahili poem and Arabic will be discussed in this document And the styles used in the two languages explained.

## **SIFA MAJUMUI ZA SHUJAA WA KIUTENDI WA KIAFRIKA**

### **Ikisiri**

Ushujaa ni dhana muhimu katika jamii yoyote ile na shujaa uonekana kuwa mkombozi wa jamii pindi jamii inapokuwa katika matatizo. Shujaa anaweza kuwa kiumbe wa kweli au wa kubuni ambaye amekuzwa na jamii au yeye mwenyewe na huwa na uwezo kuliko ule wa watu wa kawaida. Mashujaa hukumbukwa daima na hutungiwa nyimbo na tenzi kama njia ya kuwaenzi. Watafiti mbalimbali wamekuwa wakiweka msisitizo kwa shujaa mwanamume na kuwa kimya juu ya shujaa mwanamke. Ukimya juu ya shujaa mwanamke huleta picha kwamba mwanamke hawezi kuwa shujaa na ndio maana sifa ambazo zimekuwa zikianishwa na wataalamu mbalimbali kutomhusisha mwanamke. Kwani tafiti nyingi katika utendi wa Kiafrika zinaonesha kuegemea upande mmoja wa shujaa mwanamume kwa kuangalia ruwaza yake, sifa zake, anguko lake pamoja na sihiri yake. Tafiti chache ambazo zimemgusia shujaa mwanamke hazikubainisha sifa zake, hivyo, kujenga dhana kuwa sifa zinazoainishwa na wataalamu mbalimbali ndizo sifa majumui za shujaa wa kiutendi.

Lakini sifa hizo zinaleta mkanganyiko pale ambapo zinaegemea kwa mwanamume pekee ilihali kuna baadhi ya watafiti wanaomuona mwanamke kama shujaa. Makala haya yanachunguza shujaa mwanamke na shujaa mwanamume katika tendi za Kiafrika ili kubaini sifa jumui za shujaa wa kiutendi ambazo zitamjumuisha mwanamke. Makala haya yanafanya ulinganishi kati ya shujaa mwanamume na shujaa mwanamke katika utendi wa Kiafrika ili kuibua sifa jumui za shujaa wa utendi wa Kiafrika ambazo zinaweza kuwajumuisha wote yaani mwanamke na mwanamume. Makala haya yatakuwa na sehemu tano muhimu Sehemu ya kwanza inahusu kueleza sifa za shujaa mwanamume. Sehemu ya pili inahusu kubainisha sifa za shujaa mwanamke. Sehemu ya tatu inahusu kufanya ulinganishi kati ya sifa za shujaa mwanamke na shujaa mwanamume. Sehemu ya nne inahusu sifa majumui za shujaa wa kiutendi wa Kiafrika. Sehemu ya tano ni hitimisho.

Kezilahabi, Euphrase • University of Botswana, Botswana  
kezilaha@mopipi.ub.bw

## **INTERFACE BETWEEN SWAHILI AND ETHNIC ORAL LITERATURES IN TANZANIA: A PRELIMINARY OBSERVATION**

### **Abstract**

The paper discusses the mutant nature of oral literature in Tanzania and traces its development from a centrally performative art to a predominantly listener/reader audience orientation. It also touches on its seemingly surrender to the power of the media particularly the video and WhatsApps that have revolutionised critical thinking beyond class borders. To achieve this the paper looks at the problematics of writing, genres classification, interfaces of power and gender relations, the National question, global and glocal encounters, the validity of the existence of world views and the pursuit of essences. Case studies will be drawn from the northern ethnic groups of Tanzania such as: *Basukuma, Banyamwezi, Bakerebe, Bajita* and *Bahaya*. The basic question will be “quo vadis?”

### **Ikisiri**

Makala yanajadili myambuliko wa Fassihi-simulizi nchini Tanzania na yanafuatilia maaendeleo yake toka mwenendo wa uigizaji hadi ilipochukua zaidi mwelekeo wa usikilizaji na usomaji. Yanagusia pia kushindwa kwake katika kuhiimili nguvu za vyombo vya habari hasa video na *WhatsApp*s ambazo zimeleta mapinduzi ya fikra zivukazo mipaka ya tabaka. Kufanikisha mawazo haya makala yanatazama utata wa uhusiano uliomo katika uandishi, uainishaji wa mwingiliano kiuhusiano katika mamlaka ya kijinsia, suala la utaifa, utandawazi na “{utandandani”, uhakika wa kuwako kwa mtazamo wa kilimwengu na ufuatiliaji wa viini vya utu. Mifano itatolewa kutoka kwenye lugha za : Kisukuma Kinyamwezi, Kikerewe, Kijita na Kihaya. Swali linalojitokeza ni “tunakwenda wapi?”

## THE TRIPLEX MUNDUS IN EUPHRASE KEZILAHABI'S *ROSA MISTIKA*

### Abstract

Euphrase Kezilahabi purposefully ends his first controversial novella of *Rosa Mistika* (1971), the *Mystical Rose*) by foregrounding triple fateful tragedies of his *triune* characters: Zakaria—the violent and drunken father, Regina—the tenderly and hapless mother, and Rosa—the naïve turned sully daughter. Kezilahabi provides a hint to his readers of the mystique interpretation of their *three* faces of death, as enigmatically embodying *three* metaphysical secrets of life, love and parenthood. Such three dimensional alert makes an interesting case analysis of his employment of threesome motifs parodically linked to the Kerewe and biblical metanarrative to enrich his intractable subject of transcendental death that has long been lingering in existential imaginaries. I argue that Euphrase Kezilahabi, is aesthetically tangling threesome symbolism, based on two triplex categories, I term as *the implicit triple iteration* or ‘triangulation’ and *the explicit three-stage narration process*) or ‘incremental’ ; Firstly as entry point to the Kerewe culture which has evolved overtime through cross-cultural exchanges in particular with influence of western Catholicism. Secondly, as a way to prepare his readers to tragic endings of his triune characters and Kerewe traditions in general. And finally to reinforce tragic and painful memories, as brain tend to suppress sad events, like humiliation, blood spilling or death by retelling, or subsequent reiterating a text, concept or activity in new contexts. Interestingly and insightfully the pervasiveness of the trilogical or triplex symbolism is noticeable not only in Kerewe customs but as well as in several archaic and modern world cultures. I place Euphrase Kezilahabi among “gap fillers” of the emerging field of mathematical symbolization and creative literature (Smith, 1950, 1958, Glaz, 2010, 2011) to explicate the Pythagoras’s theorem that everything can be mathematically interpreted, including the novella *Rosa Mistika*.

### References

- Glaz, Sarah. 2010. Poetry Inspired by Mathematics, Proceedings of Bridges 2010, 35 – 42.
- Glaz, Sarah. 2011. “The Poetry of Prime Numbers” in the Proceedings of Bridges Coimbra, 2011:17–24.
- Kezilahabi, Euphrase. (1988). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau. (1<sup>st</sup> publication 1971).
- Smith, David. (1951, 1958). *History of Mathematics Volume 1 & II*, New York: Dover Publications.

Koenings, Nathalie A. • Hampshire College (Massachusetts), USA  
nkoenings@gmail.com

**MAZIWA HAYAUZWI: FOOD AS HISTORY AND CRITIQUE  
IN TWENTIETH CENTURY PEMBA, ZANZIBAR**

**Abstract**

This paper explores the ways that elders in Pemba talk about food and how it has changed in their lifetime. Talk about food in Pemba is a way of organizing history, as well as of assessing changes in personal agency. Elders' talk, in particular, illuminates how many people in Pemba materially experienced the 20th century – a time about which not much has been written. Talk about food, through discussions about how it should be prepared, is also a site of theorizing about the importance of time in revealing the true and best nature of things. The concept of '*\*ku-iva\**', or 'cooking through,' that emerges is a key element of elders' assessments of social health as well as powerful comment on environmental change. Central to this discourse is the figure of the *\*chungu*, *\*the clay cooking pot* – and its recent defeat by the *\*dishi*, *\*aluminum cooking pot* – talk about which provides a way of understanding many elder Pembans' views on modernity and change.

Kresse, Kai • Columbia University (New York), USA  
kaikresse@yahoo.com

## **ELIMIKA NA STAMBULI: DISCURSIVE AGENCY AND INTELLECTUAL PRACTICE ON A SWAHILI ISLAMIC RADIO SHOW**

### **Abstract**

This talk discusses an educational live on-air radio program of the first Islamic radio station on Kenya's coast in the post-Independence period, Radio Rahma in Mombasa. While Radio Rahma started broadcasting in 2004, the program 'Elimika na Stambuli' began in 2005. It was dedicated to giving voice to ordinary people's discontents about regional and national politics, their concerns about issues of piety and proper behaviour, and more, providing a public and accessible space for common reflection, discussion and critique. My paper seeks to convey a sense of the social value of the public discursive space that was created here by both makers and callers of the show in communicative interaction, as even the most difficult topics were addressed. In conclusion, I reflect on my own narrative perspective, and I discuss aspects of ethical commitment within mutual interaction (and verbal expressions used), by local Swahili speakers and radio makers as well as myself, thus exploring different layers of discursive agency that are involved here.

Lyimo, Edith B. • Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania  
edithbalyimo@yahoo.co.uk

## **FASIRI YA LUGHA KATIKA FASIHI YA ANDISHI YA WATOTO: UCHUNGUZI WA PICHA NA VIELELEZO**

### **Ikisiri**

Mtoto mdogo au mtu ambaye hajapata bado fursa ya kufundishwa herufi, hukutana na picha na vielelzo katika vitabu anavyopatiwa. Ikiwa mtoto au mtu huyu atapata kitabu chenye picha atawezu kuzielewa kwa urahisi na pengine kuzitafsiri vizuri kama zinahusiana na mazingira yake. Kwa njia hii atawezu kuelewa, kuelezea na pia kubuni mambo mengine zaidi kutokana na picha na vielelezo hivyo. Picha kama wanavyobainisha wataalamu wa vitabu vya watoto ni njia ya awali ya ujifunzaji kwa mtoto. Aidha, wataalamu walioshughulikia fasihi andishi ya watoto wanaeleza kuwa picha na vielelezo ndivyo vinavyomsaidia mtoto kuelewa kusudiao la mwandishi na pia kumpatia mlengwa (mtoto) maarifa licha ya dhima yake kuu ya kuburudisha (Ngugi 2011, Herman, 2011, Lyimo, 2014 kwa kuwataja wachache). Wataalamu hawa na wengineo wanathibitisha kupitia tafiti zao kuwa, moja ya kaida au nduni za fasihi ya watoto, hususan fasihi andishi, ni matumizi makubwa ya picha na vielelezo na kwa mujibu wa wataalamu kama vile Ruth (2015), watu wanapaswa kujifunza lugha inayowasilishwa na picha katika vitabu vya watoto. Baadhi ya maswali ambayo yanaibuliwa kama chanzo cha makala hii ni pamoja na haya yafuatayo: Je, nini maana ya lugha katika vitabu vya watoto? Je, picha ni sehemu ya lugha au lugha ni sehemu ya picha? Nini dhima ya picha na vielelezo katika fasihi andishi ya watoto? Makala hii itajaribu kujibu maswali haya kwa kuchunguza fasiri ya lugha na dhima yake katika vitabu vya watoto; na kubainisha dhima ya picha na vielelezo katika vitabu hivyo.

Mahenge, Elizabeth G. • Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania  
lizmahenge@gmail.com

## **ULEMAVU KATIKA FILAMU YA KISWAHILI: UCHAMBUZI WA LUGHA**

### **Ikisiri**

Kwa miaka ya hivi karibuni filamu ya Kiswahili imeanza kusawiri dhamira ya ulemavu ikilinganishwa na kumbo zingine za fasihi hii. Mathalani katika tamthiliya, hadithi fupi, riwaya na ushairi, dhamira ya ulemavu si ngeni ikilinganishwa na filamu ya Kiswahili. Kwa nini hali iko hivyo? Ulemavu katika makala haya unachukuliwa kuwa ni changamoto za kimaumbile alizonazo mtu pamoja na mitazamo ya wanajamii juu yake (fasili ni ya mtafiti). Nadharia ya narratolojia itatumika kuchambua ulemavu kupitia kipengele cha lugha kama kinavyojitokeza katika filamu ya MADHILA. Tutadondo baadhi tu ya sehemu kwa ajili ya kutimiza kusudi la kazi yetu. Kwa kutumia nadharia ya hii, makala yanachambua ni kwa vipi watanzi wa filamu wameisimulia hadithi ya ulemavu. Kwa umahususi, makala inataka kujibu maswali matatu ambayo ni: ni kwa vipi filamu ni fasihi? Kwa vipi lugha ya wanadamu na ya kifilamu zinafanana? Ulemavu unasimuliwaje katika filamu hii? Makala haya yanajaribu kutafuta majibu ya maswali haya.

## **DISABILITY IN KISWAHILI FILM: LANGUAGE ANALYSIS**

### **Abstract**

Recently disability issues have been portrayed in Kiswahili films as compared to other Kiswahili genres. For instance, in plays, short stories, poetry and novel disability theme is not a novel idea. Why and what happened? Disability in this paper is considered to be bodily challenges an individual has together with societal attitudes towards him or her (coined definition by researcher). Using narratology theory, the paper examines how Kiswahili film makers have portrayed disability theme in *Madhila* film. In particular, the paper attempts to address and find answers to the following queries: How is film a literature? To what extent human language equals filmic language? This paper will try to find answers to these questions.

Malonga, Pacifique • Université Nationale du Rwanda, Rwanda  
malongagitore@yahoo.com

## **THE ROLE OF KISWAHILI LANGUAGE TOWARDS FASTER INTEGRATION OF RWANDA IN THE EAST AFRICAN COMMUNITY (EAC)**

### **Abstract**

The East African Community (EAC) comprises six countries including: Burundi, Kenya, Rwanda, South Sudan, Tanzania and Uganda with a growing demand of many other regional countries applying to join. This community is believed to be the fastest growing compared to other African groups with a population of about 150 million people. With different historical backgrounds, Rwanda is the smallest country in the community and the least Kiswahili speaking due to its history. As the former Deutch Oest African together with Urundi (Burundi) and Tanganyika (now Tanzania) from 1897 to 1917 under the Germany protectorate, when Kiswahili was produced in Rwanda and later to suffer a terrible blow from the subsequent colonialist Belgium regimes and mainly catholic priests, Rwanda is now once again embracing and embarking on the development, promotion and use of Kiswahili for its faster integration and exchange in the East African Community adopting Kiswahili as its fourth official language. For its social, political and economic development, Rwanda adopted English as a medium of communication and diplomatic means of the Commonwealth and now Kiswahili as an identity a common socio-political denominator among East Africans and Africans in general for faster and sustainable communication, business, trade, exchange and political federation and understanding among EAC member states and beyond. Following this legal status of Kiswahili in Rwanda since October 2016, several steps have been taken with now the setting and creation of various associations newly formed such as: 1. Rwanda Kiswahili journalists association (WAKIRWA) 2. Rwanda Kiswahili higher learning Institutions lecturers (chama cha idara za Kiswahili vyuo vikuu Rwanda) 3. Rwanda Kiswahili university students association (CHAWAKIRWA) and 4. Rwanda Kiswahili secondary schools teachers association (CHAWAKISERWA). With the expected creation and set up of Rwanda National Kiswahili Commission, there is no doubt that Kiswahili with the help of well wishers and stakeholders, Rwanda shall achieve its objectives of developing and using Kiswahili among its citizens, the community and region as a whole. Prof Pacifique MALONGA, a well known Kiswahili specialist & promoter in Rwanda using his experience, knowledge and competence from his regional and cosmopolitan background has been involved in his voluntary and benevolent mission for over eight (8) years now since Rwanda joined EAC in 2008 and calls for your collaboration and assistance to make his dream come true. "Where there is a will there is a way". Prof Pacifique MALONGA, is a Rwandan writer and freelance journalist.

Mbarouk, Saade S. • Sumait University Zanzibar, Tanzania  
saade.mbarouk02@gmail.com

## **MAWASILIANO NA USEMEZANO KATIKA KANGA NA ATHARI ZAKE**

### **Iksiri**

Makala itazungumzia namna mawasiliano na usemezano katika kanga vinavyoleta athari tafauti katika utamaduni wa jamii ya waswahili. Vitu vingi ikiwemo kanga hutumia semi kama sehemu ya mawasiliano. Kama ilivyo aina nyengine za nguo, kanga ni moja ya vazi la utamaduni, ambalo matumizi yake makuu ni kuvaliwa. Vazi hili hutumika zaidi kwa wanawake katika maeneo ya Afrika Mashariki na hasa maeneo ya mwambao, likiwa ni vazi lao maarufu wanapo kuwa katika shughuli mbalimbali za kila siku. lakini mbali ya kuwa ni vazi la kawaida mara nyingi kanga hubeba semi maalum. Semi hizo zinaweza kuwa methali, misemo, simo na nyenginezo. Semi hizo husimamia nafasi ya mawasiliano na usemezano ambao huleta athari maalumu kutokana na tafsiri ya msomaji au mpokeaji ya mawasiliano hayo, ikiambatana na lengo la mvaaji. Pia zinakuwa na dhima mahasusi kama kuelimisha, kuonya, kuosoa, kushajiisha na kuchochea kutegemea na muktadha aliokusudia muanzishaji wa mawasiliano hayo na mpokeaji.

Mboya, Michael T. • Moi University (Eldoret), Kenya  
University of the Witwatersrand, South Africa  
[tommichaelmboya@gmail.com](mailto:tommichaelmboya@gmail.com)

**'BROKEN' KISWAHILI, "TRIBE" AND THE IMAGINATION OF THE KENYA OF  
THE FIRST DECADE OF THE TWENTY-FIRST CENTURY IN "KHANDPAKA" BY  
AWILLO MIKE AND JA-MNAZI AFRIKA**

**Abstract**

This paper brings a thick description of the political context of the time of the production of the popular song “Khandpaka” (2009) by the Kenyan music group Awillo Mike and Ja–Mnazi Afrika to bear on the reading of the song as a rhetorical act that argued for the inclusion of “tribe” in the imagination of the nation in the Kenya of the first decade of the twenty–first century. The paper’s focus is on the ironical presentation of a humorous story in “Khandpaka”. The paper amplifies the song’s critique of this narrative. It shows that the narrative, which is delivered in ‘broken’ Kiswahili, is a conflicted attempt by a fictional narrator to imagine a Kenyan nation by suppressing “tribe”. “Khandpaka” is thus read to make its argument by drawing attention to the “limitations” of the narrator’s attempt to exclude “tribe” from the imagination of the Kenyan nation.

**Keywords**

“Khandpaka”, Awillo Mike and Ja–Mnazi Afrika, Kenyan popular music, narrative, the “tribalized” politics of Kenya.

**UBAYA WANGU HAUSEMEKI: DHANA YA UNHEIMLICHE YA FREUD KATIKA  
MASHETANI YA EBRAHIM HUSSEIN**

**Ikisiri**

Lengo la makala hii ni kuchambua mhusika na dhana yenewe ya ‘Shetani’ katika tamthilia ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein. Mkabala utakaojaribu kutumika hapa unazingatia hususan uhusiano baina ya wahusika wa Shetani na Binadamu kufuatana na dhana ya Kifreud ya *Unheimliche*, iliyo na maana ya tukio ambalo si la kawaida wala lisiloelewaka na litialo hofu na wasiwasi. Uhusiano wa Shetani na Binadamu, katika fasiri hii, unakuja kuwa mfano wa uhusiano baina ya wahusika wa Juma na Kitaru kwa kiwango kidogo, na baina yao na historia kwa kiwango kikubwa. Kufuatana na dhana ya *Unheimliche* na jinsi inavyoingia katika tamthilia hii, Shetani ataonwa kama mhusika mwenye kutisha na kutia hofu. Huu mbinu si bila ya maana au umuhimu: ni ufunguo wa mtazamo huu, ambao unaeleza jinsi historia inavyoathiri binadamu na kama athari yake inakubaliwa siku zote.

**Abstract**

The purpose of this paper is to look at the character and the concept itself of the ‘Shetani’ in Ebrahim Hussein’s work *Mashetani*. The approach which will be tried here considers especially the relationship between the characters of Shetani and Binadamu according to the Freudian concept of *Unheimliche*, that, among its many meanings, has got the one of “Uncanny”. Shetani and Binadamu’s interrelation, in this interpretation, will be the representation of the relationship between the characters of Juma and Kitaru on a smaller level, and between them and History on a bigger one. According to the concept of *Unheimliche* and its role in this piece, Shetani will be seen as a scary and frightening character. This feature is not lacking of sense and importance: it’s the key to this approach, which explains how history influences men and whether its influence is always accepted.

Mnenuka, Angelus • University of Leipzig, Germany  
amnenuka@gmail.com

**BENA-SWAHILI METROLINGUAL RELATIONS IN THE BENA ORATURE:  
THE INTERFACE BETWEEN LANGUAGE AND LITERATURE**

**Abstract**

The relationship between language and literature is complex in such a way that any theoretically recognised literary text can be presented in any language when good artistic translation is made. Besides being translated earlier by philologists and anthropologists, oral literary texts could scarcely be translated without substantial loss of its content and form if no detailed socio-historical, political, and economic information is made readily available. Since it is assumed that orature is a situated social communication as maintained by Bauman (1984; 2011; 2012), using different languages other than that used by a society needs some explanations. This presentation, therefore, endeavours to discuss how Swahili and Bena languages are metrolingually employed to fulfil several stylistic functions, which, in turn, reveal how Bena people associate the Swahili language with other sociohistorical phenomena.

Morango, Alphonse B. • Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania  
bonniea2006@yahoo.com

## **MAMBO YANAYOWEZA KUSABABISHA MABADILIKO YA MAANA KATIKA SENTENSI: MIFANO KUTOKA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI**

### **Ikisiri**

Sentensi ndiyo kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo katika sintaksia chenye maana kamili na chenye vipashio vingine vidogo vya kimuundo. Pamoja na sentensi kulenga kufikisha taarifa yenyе maana kamili, wakati mwingine maana hiyo ya sentensi hubadilika. Ni dhahiri kuna vitu vinavyoweza kusababisha badiliko la maana katika sentensi. Makala haya yanabainisha na kufafanua mambo yanayoweza kusababisha sentensi kubadili maana yake na kupata maana mpya. Uchambuzi wa mambo yanayosababisha badiliko la maana yanaongozwa na nadharia ya muundo taarifa (information structure theory) kama ilivyoadisiwa katika shule ya Prague (1966) kama ilivyofafanuliwa na Danes (1966). Ufafanuzi wa nadharia hii umejikita katika tofauti za miundo zinazosababisha taarifa zenyе maana tofauti kisemantiki. Katika Nadharia hii inaaminika kuwa, miundo mbalimbali ya sentensi huweza kuchanuza maana tofauti za sentensi, kadri unavyobadilisha maneno au mpangilio wa sentensi, unaunda miundo tofauti ya sentensi yenyе maana tofauti. Makala yametumia data zilizopatikana kutoka maktabani. Makala haya yamebaini mambo mbalimbali yanayoweza kusababisha sentensi kubadili maana. Mambo hayo yanaweza kuwa, lengo, kategoria za kisarufi, uhusiano wa viambajengo, mkazo, uhisisvu, umada, kiimbo, mpangilio, na kadhalika. Makala haya yamegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni utangulizi, ambapo dhana ya sentensi imefasiliwa, kiini, kinachofafanua namna sentensi zinavyobadili maana kulingana na mambo mbalimbali na mwisho ni hitimisho lililotoa ufupisho wa makala na mapendekezo.

### **THINGS THAT MAY CAUSE CHANGES OF MEANINGS IN A SENTENCE: EXAMPLES FROM KISWAHILI LANGUAGE**

#### **Abstract**

A sentence is the larger structural constituency in the sentence that convey the meaning and it has other small constituencies. Despite of the sentence focusing on conveying the meaning, sometimes the meaning changes. It is obvious that there are things that may cause changes of meaning in the sentence

. The article expresses things that may cause the sentence to change its meaning and gain a new one. Analysis on the changes of meaning are led by the Information Structure Theory pioneered in the prague school 1966 as expressed by Danes in the same year. The theory expresses different structures that give different sentence meanings. The theory believes that various sentence structures extend different sentence meanings as it changes words or sentence order. The article has used the data from the library. Various things that may cause sentence meanings have been discussed such as focus, structural categories, constituency relations, stress, topicalization, word order etc. The article is divided into three parts; introduction, which defines the sentence, the body which portray things which change the sentence meaning and last, conclusionwhich gives the article summary and suggestions.

Msigwa, Arnold B.G. • Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania  
agawasike@gmail.com

**CHANGAMOTO ZA ISTILAHİ KATIKA UANDISHI WA  
TASINIFU ZA UZAMILI WA KISWAHILI TANZANIA**

**Ikisiri**

Uthabiti wa taasisi yoyote ya elimu ya juu hasa katika ngazi ya Chuo Kikuu unatokana na uimara wa programu zitolewazo katika taasisi husika na ubora wa wahitimu katika ngazi husika. Kuimarika kwa programu kama za Umahiri na Uzamivu ni sifa mojawapo ya taasisi ya elimu ya juu. Kuimarika huko hakutawezekana kama eneo la istilahi za kitaaluma zinazotumika kwa uwanja husika isimu/fasihi na methodolojia ya utafiti hazitakuwa sanifu na thabiti. Hivyo, makala haya yanafafanua changamoto za kistilahi katika programu za M.A. (Kiswahili) na PhD (Kiswahili) katika TATAKI kwa uzoefu wa miaka mitano. Swali linaloibuliwa na makala haya ni je, kutakuwa na usanifu wa program kama usanifishaji wa istilahi haujafanywa na taasisi husika. Mwito wa makala haya kwa watawala wa TATAKI na Chuo Kikuu kwa ujumla wake, ni kwamba, hima usanifishaji wa Istilahi katika Kiswahili hasa katika eneo la methodolojia ufanyike haraka kabla jahazi kuzama.

Mutembei, Aldin K. • Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania  
mutembei@yahoo.com

## **USHAIRI WA KISWAHILI ULIKOTOKA NA UNAKOELEKEA: MAJAGINA WA USHAIRI KATIKA WHATSAPP NI MCHANGO AU CHANGAMOTO?**

### **Ikisiri**

Mwishoni mwa miaka ya 1960 wataalamu wa ushairi wa Kiswahili waliingia katika malumbano makali. Yaliyoanza kama mazungumzo ya kawaida mara yalizoa ugomvi mkali. Katika taaluma, ikajitokeza dhana ya “mgogoro” wa ushairi wa Kiswahili. Ingawa “mgogoro” huo umepoa, ni kama volkano hai inayoweza kulipuka wakati wowote. Kwa upande mwingine, kukolea kwa matumizi ya mitandao ya kijamii kumetokeza chachu mpya katika historia ya ushairi wa Kiswahili. Mtandao wa mawasiliano wa Whatsapp ni mfano wa pekee ambao ama unatoa mchango au changamoto katika historia ya ushairi wa Kiswahili. Katika mtandao huo makundi mawili lile la Wakita Afrika (Wafia Kiswahili-Afrika) lililoanzishwa tarehe 31 Julai 2015; na lile la Majagina wa Ushairi lililoanzishwa tarehe 27 Disemba 2014, yamekusanya kwa pamoja washairi mbalimbali kutoka Afrika mashariki na kuwafanya walumbane, watumiane salamu, wachokozane, wataniane, waonyane nap engine kusifiana yote hayo wakiyapitisha katika mtindo na maumbo changamani ya mashairi ya Kiswahili. Makala hii imefuatilia ujitokezaji wa mitindo, maumbo na namna mbalimbali za mawasiliano kuitia katika mashairi ya makundi haya mawili. Swali tunalojiuliza, je ushairi wa Kiswahili unapiga hatua? Je, jamii ya Waswahili iwe tayari kupokea tena mgogoro wa aina nyingine katika ushairi wa Kiswahili au hatua hii ni ya kupongeza? Katika makala hii, nadharia ambayo inakidhi hali inayojitokeza sasa katika ushairi ni ile ya mwingiliano matini. Hata hivyo, makala hii ni ya kiuchokozi ikitoa maswali mengi kuliko majibu.

Mwangovya, Joan A. • Karatina University, Kenya  
janzazi@karu.ac.ke

## A COMPARATIVE ANALYSIS OF THE GERMAN AND SWAHILI LANGUAGES OF CORRUPTION

### Abstract

The paper aims at doing a contrastive analysis of the language of corruption as portrayed in the German language and the Kiswahili language. Corruption as an emerging issue in Kenya has been a thorny issue in the recent years that has plagued the country and has led to the collapse of essential institutions. The clamour for the sacking of high-profile and well to do figures in Kenya indicates that the populace are tired of this menace and they would like to see a change in as far as curbing this vice is concerned. This issue is not only a plague in Kenya but also in other developed countries. This paper would highlight instances of corruption cases as portrayed in the two languages like German and Kiswahili. This would be a comparative study to see how this issue is solved either at individual level or collectively. as a country has also had its fair share of scandals and despite the fact that the country is considered devoid of such vices, they too have had to tackle this vice. Moreover corruption has a face and a language, and one may be tempted to ask, what the language of corruption? In the Kiswahili language we have a number of sayings and proverbs that are used to ask for and receive bribes. The German language has a number of sayings and proverbs that are used in expressing the intention of the speaker to give and to receive bribes. This paper aims at taking a keen interest on these sayings and proverbs used in corruption, with a view of drawing out the similarities and differences. Over and above that it seeks to find out how the two cultures and countries differ in their perspective of corruption, and how language as a tool has been used to perpetuate corruption in the respective countries.

Nassenstein, Nico • University of Cologne, Germany• nnassenstein@aol.com  
Bose, Paulin B. • Uganda Christian University, Kampala • bose.baraka0@gmail.com

## **CONTACT-INDUCED FEATURES OF KIVU SWAHILI (DR CONGO)**

### **Abstract**

In more recent studies (Nassenstein & Bose 2016, Bose & Nassenstein 2016) Kivu Swahili has been described as a Swahili regiolect that can be clearly differentiated from the Swahili(s) spoken in Lubumbashi/Katanga, Kisangani/Tshopo and Bunia/Ituri (all DR Congo), revealing salient features in noun and verb morphology that are not found elsewhere. The present contribution aims to discuss contact-induced features of this variety, taking lexical and structural examples of borrowing, calquing and metatypy into account. Language contact in the multilingual landscape of the Kivus reveals a certain degree of divergence in terms of the current realization of Kivu Swahili as spoken in Goma, North Kivu province, and Bukavu, South Kivu province, due to speakers' different group languages. While in North Kivu, especially Kinyabwisha and Kinande have had an impact on the language, in South Kivu predominantly Mashi and Kilega have shaped the specific realization of Swahili found on-site. Other languages such as French or Lingala that have – lexically and structurally – largely contributed to the present form of the language are not bound to one area or group of speakers. The suggested talk eventually raises the question whether a specific realization of Kivu Swahili with more or less contact features (such as a large amount of Lingala lexicon, more or less Kinyabwisha/Kinande morphology etc.) gives birth to ethnic registers of Kivu Swahili that serve different social purposes such as in-group status, intimidation, protection or deliberate exclusion, when analyzed against the background of the ongoing conflict in the area.

### **References**

- BOSE, Paulin Baraka & Nico Nassenstein. 2016. Morphosyntactic core features of Kivu
- Swahili: A synopsis. Afrikanistik & Ägyptologie Online (AAeO) 2016. [<https://www.afrikanistik-aegyptologie-online.de> ]
- NASSENSTEIN, Nico & Paulin Baraka Bose. 2016. Kivu Swahili texts and grammar notes.
- Munich: LINCOM.

## **DHANA YA UCHAWI KATIKA KAZI ZA SANAA: MIFANO KUTOKA MUZIKI WA KIZAZI KIPYA, MZEE WA BUSARA NA KAFARA**

### **Ikisiri**

Uchawi ni fani maarufu imekuwepo ulimwenguni kwa muda mrefu sana. Wapo wanaoutazama uchawi kama jambo zuri na lenye kufaa kwa ustawi wa binadamu. Wengine wanauona uchawi kama jambo la hovyo na linalotishia ustawi wa mwandamu. Jambo la muhimu hapa ni kuwa pande zote mbili zinakubali na kukiri uwepo wa fani hii katika maisha yetu ya kila siku. Mionganini mwa watafiti wa mwanzo kuchunguza dhana hii ni J. Middleton na E. H. Winter (1963), wao waliona kuwa dhana ya uchawi inajumuisha uzuri na ubaya katika jamii ya Waafrika. Tafiti nyingi zilizojikita katika kuchunguza kuhusu ufaafu au kutofaa kwa fani ya uchawi katika bara la Afrika zimefanyika kuanzia miaka ya sitini. Mionganini mwa tafiti za hivi karibuni kabisa ni pamoja na Zande (1995), Douglas (1973), Geschiere (2000), Bond na Ciekawy (2001), Wamitila (2002), Khamisi (2005), Bernault (2006) na Walibora (2010).

Wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipywa kama sehemu ya wanajamii nao wanautazama uchawi kwa jicho la kisanaa. Wapo wanaoshadadia ufaafu wa fani hii lakini pia wapo wengi wanautazama fani hii kama mila potofu na inayopaswa kupigwa vita kwa hali na mali. Hivyo makala haya yanalenga kuchambua mtazamo wa wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipywa kuhusu dhana ya uchawi. Tutajikita katika kujadili dhana yenye ya uchawi kwa namna inavyojitokeza katika muziki wa kizazi kipywa, mtazamo wa wasanii kuhusu namna na aina ya uchawi unavyojidhihirisha katika jamii zao na mwishoni tutajadili mtazamo wa wasanii kuhusu athari za uchawi katika jamii, kwa sehemu kubwa makala yetu itaongozwa na nadharia ya *Uhalisiamazengaombwe*.

Istilahi muhimu ni uchawi, Sanaa na Muziki wa Kizazi Kipywa

Nicolini, Cristina • Chuo Kikuu cha Napoli, Italy  
christina.nicolini@gmail.com

## **ULINGANISHAJI BAINA YA LUGHA YA UNYAGO NA LUGHA YA MABANGO DHIDI YA UKIMWI KATIKA TANZANIA LEO**

### **Ikisiri**

Makala haya yanalenga kuchunguza kwa mtazamo linganishi kufanana, kutofautiana na kuhusiana baina ya mafunzo yanayotolewa kwa mwali kupitia nyimbo za unyagoni na maandishi ya tahadhari yanayotumika katika njia za mawasiliano ya kisasa, kama mabango au michoro ya ukutani, inayotumiwa na miradi ya serikali pamoja na asasi zisizo za kiserikali katika kinga dhidi ya VVU/UKIMWI. Lengo la kwanza ni kuchambua mifumo, mitindo na mikakati ya miviga, hasa unyago, ambao ni “taasisi ya mafuzo mbalimbali”, inavyorithiwa kupitia kwa maendeleo ya mawasiliano kama aina ya uwasilishaji wa ujumbe wa kinga dhidi ya VVU/UKIMWI. Lengo jingine ni kuchanganua jinsi ilivyobadilishwa nyimbo za unyago za kisasa ili zihamasishe na kuwafundisha wasichana watanzania kuhusu magonjwa ya zinaa yakiwemo VVU/UKIMWI. Dhamira kuu ya kazi hii ni ulinganishi wa lugha zinazohusu elimu dhidi ya VVU/UKIMWI. Kwa upande mmoja ninajadili mbinu za mapokeo za jadi katika kuwasilisha ujumbe wa elimu na maadili kuhusu VVU/UKIMWI - nikichunguza mapokeo kupitia katika nyimbo za unyagoni – na upande mwengine ninajadili vita dhidi ya ugonjwa wa VVU/UKIMWI katika njia za kisasa za mawasiliano, hasa lugha kwenye mabango nchini Tanzania. Katika mjadala huu nitatumia nadharia ya Mwingiliano matini (Intertextuality) na nadharia ya Socholojia ili kuyaeleza hayo niliyoyatafiti.

### **Abstract**

This article aims to investigate with a comparative perspective the similarities and the linkages or relationships between the teachings given to the young initiate through the traditional songs of the female initiation rite of *unyago* and the warning text exploited in the modern ways of communication, as billboard, posters and murales, used for the prevention of HIV / AIDS by international NGOs and local government projects. The first objective is to analyze the codes, styles and techniques of the traditional rituals, especially the rite of passage of *unyago*, that is indeed a “department of various teachings”, passing through the development of the communication, as a way to spread a prevention message against HIV / AIDS. Another goal is to analyze how are changing the modern songs of *unyago*

to inform and teach the Tanzanian girls about the spread of STI'S (sexually transmitted infections) including HIV / AIDS. The leitmotiv of this work is to make a comparison between different "languages" about the knowledge against HIV/AIDS. On one hand I will discuss the tools inherited from the traditional cultural substratum in conveying an educational message about HIV/AIDS – particularly analyzing the customs and the language inherited from the songs of *unyago*, on the other hand I will analyze the fight against the spread of HIV / AIDS in the contemporary forms of communication, especially the language of billboards in Tanzania. In this paper I will utilize, to explain my research, the theory of Intertextuality in a social perspective.

Nieber, Hanna • Zentrum Moderner Orient  
Berlin Graduate School Muslim Cultures and Societies, Germany  
Nieber@bgsmcs.fu-berlin.de

## **WRITING “WRITING” FROM THE SWAHILI COAST INTO ANGLOGRAPHIC ACADEMIA**

### **Abstract**

